# PDPC FARAGHA NEWSLETTER

Toleo Na. 0004 Oktoba - Desemba 2025

# PDPC NA NHIF KUIMARISHA USHIRIKIANO KATIKA KULINDA FARAGHA NA TAARIFA BINAFSI ZA WANACHAMA.

Dkt. Mkilia alisisitiza kuwa ushirikiano huo ni muhimu. **HABARI KAMILI UK. 03**




Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia (Kulia) na Makamu Mkuu wa Chuo kikuu Huria Tanzania (OUT), Prof. Alex Makulilo, (Kushuto) wakibadilishana hati ya maridhiano ya kutoa Ithibati kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPO's). **HABARI KAMILI UK. 05**

## DPOs WAIPONGEZA PDPC KWA KUWAJENGEA UWEZO KATIKA ULINZI WA TAARIFA

Wamesema mafunzo hayo yamewajengea uelewa wa kina kuhusu matakwa ya PDPA. **HABARI KAMILI UK. 12**

# YALIYOMO

03 PDPC NA NHIF KUIMARISHA USHIRIKIANO KATIKA KULINDA FARAGHA NA TAARIFA BINAFSI ZA WANACHAMA.

05 PDPC NA OUT WAJA NA MPANGO WA PAMOJA WA KUTOA ELIMU YA DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI KWA DPO's NCHINI.

07 HABARI PICHA

13 PDPC YAADHIMISHA WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA KWA KUTOA ELIMU KWA UMMA.

14 MATANGAZO

18 ELIMU YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA YAWAFIKIA PDPC

19 PDPC NA HUAWEI WALIFANYA MKUTANO WA KILELE WA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI.



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Dkt. Emmanuel Mkilia (Kushoto) akisalimiana na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) Dkt. Irene Isaka (Kulia) mara baada ya kuwasili kwenye ofisi ya NHIF jijini Dodoma mnamo Novemba 12, 2025.

# PDPC NA NHIF KUIMARISHA USHIRIKIANO KATIKA KULINDA FARAGHA NA TAARIFA BINAFSI ZA WANACHAMA.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Dkt. Emmanuel Mkilia amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) Dkt. Irene Isaka jijini Dodoma.

Mazungumzo hayo yamelenga kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili katika kulinda faragha na taarifa binafsi za wanachama wa NHIF hasa katika zama hizi za mabadiliko ya kidijitali katika utoaji wa huduma za afya.

Kupitia Sheria ya Bima ya Afya ya Taifa, NHIF ina jukumu muhimu la kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma bora na nafuu za afya.

Mfuko huo unasimamia taarifa nyeti binafsi za kiafya za mamilioni ya wananchi, hivyo usalama na uadilifu wa taarifa hizo ni msingi wa kuimarisha imani ya umma katika mifumo ya kidijitali.

Katika mazungumzo hayo Dkt. Mkilia alisisitiza kuwa, ushirikiano kati ya PDPC na NHIF ni muhimu katika kuhakikisha usimamizi wa taarifa binafsi unafanyika kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa vya faragha na usalama wa taarifa. Aliongeza kuwa juhudi za pamoja zitasaidia kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu haki zao za faragha na wajibu wa kulinda taarifa zao wanapotumia huduma za bima ya afya.



Kwa upande wake Dkt. Isaka alieleza kuwa NHIF inatekeleza mageuzi makubwa ya kidijitali yanayolenga kuboresha upatikanaji wa huduma, na kwamba ushirikiano na PDPC utasaidia kuhakikisha mifumo hiyo ni salama na inalindwa na kuaminika zaidi.

Viongozi hao walikubaliana kuwa na mpango wa pamoja wa uelimishaji wa umma. PDPC na NHIF zitashirikiana kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda taarifa zao binafsi za kiafya kupitia bima ya afya na umuhimu wa kujua hatima ya faragha za taarifa hizo.

Ushirikiano huu utasaidia kuimarisha imani ya wananchi katika mifumo ya afya na taarifa katika mifumo ya kidijitali, kukuza uwajibikaji katika usimamizi wa taarifa binafsi kwa watoa huduma na wanufaika, kusaidia utekelezaji wa ajenda ya Serikali kuhusu bima ya afya kwa wote, kuongeza uelewa na utii wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 na zile za kimataifa kuhusu faragha na ulinzi wa taarifa binafsi.

Ushirikiano huu kati ya PDPC na NHIF unatarajiwa kuwa mfano wa kuigwa katika sekta ya afya na taasisi nyingine za umma na binafsi, katika kuhakikisha Tanzania inasonga mbele kwa usalama, uwazi na uaminifu katika matumizi ya teknolojia za kidijitali katika huduma za afya zenye taarifa nyeti za wanachama.



# PDPC NA OUT WAJA NA MPANGO WA PAMOJA WA KUTOA ELIMU YA DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI KWA DPO's NCHINI.




Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia (Kulia) na Makamu Mkuu wa Chuo kikuu Huria Tanzania (OUT), Prof. Alex Makulilo (Kushoto) wakionesha hati ya maridhiano ya kutoa elimu ya dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPO's) mara baada ya kusaini hati hiyo ya miaka mitano (5) ambapo kwa pamoja wataendesha mafunzo maalumu ya DPO's na kutoa vyeti vya taaluma kupitia vituo vya OUT vilivyopo nchi nzima. Hafla hiyo ilifanyika Novemba 14, 2025. Makao makuu ya Chuo Kikuu Huria Tanzania, jijini Dar es salaam.

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) wameingia katika ushirikiano wa kimkakati kwa kusaini hati ya makubaliano inayolenga kuimarisha uelewa, weledi na utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (PDPA) kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi Nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa PDPC Dkt. Emmanuel Mkilia ameweka bayana kuwa ushirikiano huo baina ya PDPC na OUT utasaidia katika uandaaji wa maudhui yatakayowezesha Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPO's) kupata elimu sahihi kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi na kupatiwa vyeti ambayo vitawapa nafasi ya kutambulika rasmi kitaaluma.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Novemba 14, 2025 wakati wa hafla fupi ya kusaini hati ya makubaliano ya ushirikiano wa Miaka Mitano (5) kati ya PDPC na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), ambapo amesema Ulinzi wa Taarifa Binafsi ni Swala mtambuka linalohitaji utekelezaji wa hiyari kwakua jambo hilo linafaida nyingi kwenye uchumi wa kidigitali.

"PDPC ilianzishwa mwaka 2022 kwa ajili ya kulinda faragha za watu na kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi nchini. Jambo hili lina faida kubwa kwa sababu linaongeza uaminifu, usiri wa taarifa za watu na kukuza uchumi wa kidigitali unaovutia wawekezaji," amesema Dkt. Mkilia.

## “Makubaliano hayo yanalenga kujenga uwezo, kuongeza uelewa na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 unafanyika kwa viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa”

“Makubaliano hayo yanalenga kujenga uwezo, kuongeza uelewa na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 unafanyika kwa viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa ambapo kupitia makubaliano haya Chuo Kikuu Huria (OUT) wataanza kutoa mafunzo ya kitaaluma kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPOs), ili wawe na ujuzi na weledi unaohitajika katika kusimamia, kulinda na kutumia taarifa binafsi kwa usahihi ndani ya taasisi zao” alisema Dkt. Mkilia.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) Prof. Alex Makulilo ameahidi kutekeleza makubaliano hayo kwa maslahi ya umma.

“Tunapaswa kuingia kwenye utekelezaji mara moja, taifa linahitaji wataalamu wenye uwezo wa kutafsiri, kusimamia na kutekeleza sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa weledi na kwa maslahi mapana ya umma” alisema, Prof. Makulilo.

Hati hiyo ya maridhiano ya miaka mitano (5) ya kutoa elimu ya dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa (DPO’s) ili kuboresha ulinzi wa taarifa binafsi nchini imesainiwa ikiwa ni jitihada za PDPC kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi unafanyika kikamilifu na kwa usahihi.




Dkt. Emmanuel Mkilia, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) na Prof. Alex Makulilo, Makamu Mkuu wa Chuo kikuu Huria Tanzania (OUT) wakisaini hati ya maridhiano ya miaka mitano (5) ya kutoa elimu ya dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa (DPO’s) ili kuboresha Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini. Hafla hiyo ilifanyika jijini DSM, Novemba 14, 2025 kwenye Makao makuu ya OUT na kushuhudiwa na baadhi ya watumishi wa Taasisi zote mbili yaani PDPC na OUT.



## HABARI PICHA:

Ziara ya Kikazi ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki (Mb), pamoja na timu ya menejimenti ya Wizara hiyo, kwenye Ofisi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dodoma. Desemba 15, 2025.




Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki (Mb), akisaini kitabu cha Wageni mara baada ya kuwasili kwenye ofisi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dodoma. Desemba 15, 2025.





Dkt. Emmanuel Mkilia, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), akisalimiana na baadhi ya Watumishi wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, baada ya kuwasili kwenye ofisi ya PDPC) Dodoma, kwaajili ya Ziara ya Kikazi Iliyoongozwa na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki (Mb), Desemba 15, 2025.



Dkt. Emmanuel Mkilia, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi(PDPC), akiwasilisha ripoti ya Utekelezaji wa Tume kwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki (Mb), wakati wa ziara ya Kikazi ya Mhe. Waziri. Desemba15, 2025 - Dodoma.



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki (Mb), akimsikiliza Dkt. Emmanuel Mkilia, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), wakati akiwasilisha ripoti ya Utekelezaji wa Tume kwenye ziara ya Kikazi ya Mhe. Waziri. Desemba15, 2025 - Dodoma.








Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia akimkabidhi zawadi Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki (Mb). Mara baada ya kuhitimisha ziara yake ya kikazi ya siku moja kwenye Ofisi ya PDPC - Dodoma, tarehe 15 Desemba, 2025.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Mhe. Balozi Adadi Rajabu akiongoza Kikao cha saba cha Bodi hiyo ambacho kilipokea na kujadili utendaji kazi wa PDPC kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2025. Kikao hicho kilifanyika tarehe 19 Desemba 2025 katika ofisi ya PDPC - Dodoma.











Baadhi ya Wajumbe wa kikao cha Bodi ya Wakurugenzi ya PDPC, wakifatilia kwa kina Kikao cha saba cha Bodi hiyo katika ofisi ya PDPC - Dodoma.



@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz

# DPOs WAIPONGEZA PDPC KWA KUWAJENGEA UWEZO KATIKA ULINZI WA TAARIFA

Washiriki wa mafunzo maalum ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa (DPOs) wameipongeza Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kwa kuandaa na kutoa mafunzo mahususi yanayolenga kuwaongezea uwezo kwenye utendaji wao hasa katika kusimamia na kulinda taarifa binafsi ndani ya taasisi zao.

Wamesema mafunzo hayo yamewajengea uelewa wa kina kuhusu matakwa ya sheria, mbinu za kutathmini athari, na namna ya kuhakikisha taarifa za wananchi zinalindwa ipasavyo katika mfumo wa kidigitali unaokua kwa kasi.

"Mafunzo haya binafsi yamenifungua macho kuhusu umuhimu wa kuwa na mifumo madhubuti ya ulinzi wa taarifa tulizonazo kwenye kampuni yetu, na yametupa weledi wa jinsi ya kusimamia mzunguko mzima wa taarifa kuanzia ukusanyaji hadi uhifadhi. Nawapongeza sana PDPC, utayari wao wa kutoa mafunzo ya mara kwa mara ni ishara ya kujitoa katika kuhakikisha taifa linakuwa na wataalamu wenye uwezo wa kutosha kulinda taarifa binafsi" alisema Bw. Enock Helongwa, DPO wa Taasa Luxurious Lodges & Camps.

**"Naishauri PDPC kuendeleza utaratibu huu wa utoaji wa mafunzo ili kuwafikia Maafisa Ulinzi wa Taarifa wengi zaidi kwasababu Ulinzi wa Taarifa Binafsi ni eneo linalohitaji uelewa mpana ndani ya taasisi zote."**

"Naishauri PDPC kuendeleza utaratibu huu wa utoaji wa mafunzo ili kuwafikia Maafisa Ulinzi wa Taarifa wengi zaidi kwa sababu ulinzi wa taarifa binafsi ni eneo linalohitaji uelewa mpana ndani ya taasisi zote, bila kujali ukubwa au aina ya huduma inayotolewa" alisema Bi. Margaret Mhina, DPO wa C. Steinweg Bridge Tanzania Limited.

Mafunzo hayo ya siku tatu kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa (DPOs) yanalenga kuhakikisha kila taasisi nchini inakuwa na DPO mwenye ujuzi wa kutosha kutekeleza misingi ya ulinzi wa taarifa kwa kuzingatia haki, uwazi, usalama na uwajibikaji. Mafunzo yamekuwa endelevu ikiwa hii ni awamu ya tano ambapo zaidi ya DPOs, 200 wameweza kushiriki hivyo kuongeza idadi ya wataalamu wanaobobea katika fani hiyo muhimu.







Ni baadhi ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPOs) kutoka Taasisi mbalimbali nchini na nje ya nchi wakiuliza Maswali na kufuatilia mada mbalimbali zilizotolewa kwenye mafunzo maalum ya siku tatu kwa DPOs, yaliyoandaliwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kwa lengo la kuwaimarishia uwezo wa utendaji kazi wa DPOs na kuziongezea ufanisi Taasisi za umma na binafsi katika utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 na kanuni zake.




Baadhi ya watumishi wa PDPC, Ofisi ya Zanzibar wakiongozwa na Bw. Amour Abdalla Amour (wakwanza kushoto), Afisa Utawala na Rasilimali watu, na Bw. Maulid Kipevu (wa kwanza kulia), Afisa Habari, wakitoa elimu ya Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwenye ofisi ya Milele Zanzibar Foundation.

## PDPC YAADHIMISHA WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA KWA KUTOA ELIMU

Maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa wateja hufanyika kila mwaka kuanzia Oktoba 6 hadi 10, na taasisi mbalimbali hutumia wiki hii kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma wanazozitoa.

Katika kuadhimisha wiki hii kwa mwaka 2025, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) ilitembelea ofisi mbalimbali Visiwani Zanzibar kwa lengo la kuwafikia wadau na kuwapa elimu ya dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi sambamba na kuzikumbusha taasisi hizo kujisajili PDPC ili kuhakikisha ulinzi wa faragha za watu unazingatiwa katika uendeshaji wa shughuli mbalimbali nchini.

Timu hiyo kutoka PDPC iliongozwa na Bw. Amour Abdalla Amour, Afisa Utawala na Rasilimali watu, PDPC - Ofisi ya Zanzibar na Bw. Maulid Kipevu, Afisa Habari, PDPC - Ofisi ya Zanzibar.

Milele Zanzibar Foundation, The Creative Education Foundation Zanzibar na Asasi za Kiraia Zanzibar (ANGOZA) ni miongoni mwa Taasisi zilizotembelwa na kupatiwa huduma.






# MISINGI NANE (8) YA UKUSANYAJI NA UCHAKATI WA TAARIFA

kuna misingi nane (8) ya Ukusanyaji na Uchakataji wa taarifa binafsi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 **(PDPA)** na katika Kanuni za Ukusanyaji na Uchakataji wa Taarifa Binafsi.

Wakusanyaji na Wachakataji wa Taarifa Binafsi nchini wanapaswa kuzingatia Misingi hii ili kulinda faragha za wahusika wa taarifa na kuzuia matumizi mabaya ya taarifa hizo.

Kanuni namba 23 ya Kanuni za Ukusanyaji na Uchakataji wa Taarifa Binafsi imewaka wazi misingi hii, pia kwenye PDPA Kifungu cha tano (5) kimeweka bayana kuhusu misingi hii ambayo ni;-

## Haki na uwazi

Taarifa binafsi zinapaswa kukusanywa na kuchakatwa kwa njia halali, isiyo ya udanganyifu na kwa uwazi kwa muhusika wa taarifa.

## Madhumuni maalumu

Taarifa binafsi zinapaswa kukusanywa na kuchakatwa kwa madhumuni maalumu ambayo umemjulisha muhusika wa taarifa na akaridhia.

## Ufanisi na ukomo

Taarifa binafsi zinapaswa kukusanywa na kuchakatwa kwa ufanisi (relevancy) na kwa kiwango kinachohitajika tu (Data Minimization) ili kuzuia kuwa na taarifa nyingi ambazo huzitumii.

## Usahihi

Taarifa binafsi zinapaswa kukusanywa na kuchakatwa kwa usahihi, za karibuni, na hatua za kusahihisha zinapaswa kupatikana pale zinapo-bainika kuwa si sahihi.

## Usalama

Taarifa binafsi zinapaswa kukusanywa na kuchakatwa kwa usalama, pia taasisi zinazotunza taarifa hizo zinapaswa kutumia hatua za kiufundi ili kuzilinda dhidi ya upotevu, uharibifu au udukuzi.

## Uwajibikaji

Taasisi zinazokusanya na kuchakata taarifa binafsi zinapaswa kufuata kanuni zote za ulinzi wa taarifa, binafsi na zinapaswa kuwa na mifumo au sera zinayoonyesha jinsi zinavyotekeleza wajibu huo.

## Muda wa kuhifadhi

Taasisi zinazokusanya na kuchakata taarifa binafsi zinapaswa kuhifadhi taarifa kwa muda walipanga tu na baada ya muda huo wanapaswa kuzifuta au kuzisambaratisha kwa njia salama baada ya kipindi kinachoendana na madhumuni.

## Ridhaa ya Muhusika

Taarifa binafsi hazipaswi kufichuliwa kwa watu au taasisi zisizohusiana isipokuwa pale muhusika wa taarifa anapojulishwa na kuridhia au Sheria inapohitaji.


@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz

## KIDOKEZO CHA ULINZI WA TAARIFA



Kila mmoja wetu anaweza kuwa balozi wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwenye sehemu mbalimbali tunazopatiwa huduma. Iwe katika familia, katika jamii na hasa kwenye mitandao ya kijamii.





Pata huduma kwenye Taasisi/kampuni iliyosajiliwa na PDPC ili kujihakikishia usalama wa Taarifa zako unazozitoa wakati wa kupatiwa huduma husika.






#LINDA
TAARIFA
BINAFSI
TZ
TUFUATILIE
TIKTOK
@pdpc.tz
SCAN HERE • TO FOLLOW US •
SCAN HERE • TO FOLLOW US •




PDPC
TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI
TUFUATILIE
WHATS APP
@
Tume Ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi
Channel info
Tume Ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC)
Forward
Share
Karibu kwenye Channel ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Channel hii Itakuwa Ina kuleta Taarifa mbalimbali kutoka Tume.
Mute
Public channel
What you share is visible to anyone, but your phone number isn't. Tap to learn more.
Channel alerts
Channel settings



Baadhi ya Watumishi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) wakimsikiliza kwa umakini Afisa uelimishaji kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma Bw. Faustine Malecha wakati akiwapatia elimu kuhusu umuhimu wa kuzuia na kuepuka vitendo vya rushwa katika maeneo ya kazi.

# ELIMU YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA YAWAFIKIA PDPC

Afisa uelimishaji kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma Bw. Faustine Malecha, tarehe 24 Novemba, 2025 alitoa elimu kwa watumishi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kuhusu umuhimu wa kuzuia na kuepuka vitendo vya rushwa katika maeneo ya kazi.

Katika mafunzo hayo, yaliyofanyika kwenye ukumbi wa ofisi za PDPC, zilizopo Dodoma, Bw. Malecha alisisitiza kuwa rushwa si tu inashusha ufanisi wa taasisi za umma, bali pia inaathiri uaminifu wa wananchi kwa Serikali na kuhatarisha maendeleo ya Taifa.

"PDPC ni taasisi muhimu inayosimamia utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, inapaswa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma na kuhakikisha kuwa maamuzi yote yanafanywa kwa uadilifu, uwazi na haki" alisema Bw. Malecha.

Bw. Malecha pia alitoa mwongozo wa namna watumishi wanaweza kutambua viashiria vya rushwa, jinsi ya kuripoti vitendo vinavyohisiwa kuwa ni vya rushwa, na umuhimu wa kujenga utamaduni wa kuwajibika katika kila hatua ya utoaji huduma.

PDPC ina jukumu la msingi la kulinda haki ya faragha ya wananchi kwa kuhakikisha taarifa zao binafsi zinakusanywa, kuhifadhiwa na kutumika kwa mujibu wa Sheria hivyo kujenga jamii inayotumia teknolojia kwa usalama, uaminifu na kwa manufaa ya maendeleo ya taifa.





Baadhi ya Watumishi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) na Watumishi wa HUAWEI wakiwa kwenye picha ya pamoja mara baada ya kuhitimisha Mkutano wa kilele cha Ulinzi wa Faragha uliofanyika, tarehe 20 Desemba 2025 jijini Dodoma.

## PDPC NA HUAWEI WAFANYA MKUTANO WA KILELE CHA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Tarehe 20 Desemba 2025, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) na Huawei walifanya Mkutano wa Kilele cha Ulinzi wa Faragha.

Mkutano huo ulifanyika Jijini Dodoma na ulilenga kuwaleta pamoja viongozi na wataalam kutoka PDPC na Huawei kwa majadiliano ambayo yalijikita katika kuimarisha Ulinzi wa Taarifa Binafsi Nchini na kujenga ubunifu unaoendeshwa na uaminifu.

Tukio hilo lilithibitisha dhamira ya PDPC na Huawei katika kuendeleza Ulinzi wa Taarifa Binafsi, kuongeza ufahamu na kuunga mkono mipango ya Serikali inayoweka uaminifu, uwajibikaji katikati ya maendeleo ya teknolojia.



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia akizungumza na washiriki wa Mkutano wa Kilele cha Ulinzi wa Faragha.



# WASILIANA NASI

Huduma kwa wateja:

**+255753459155**
**+255736110505**
**+255718462536**
**+255744057652**
**+255615779070**

Barua pepe:

**helpdesk@pdpc.go.tz**

@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz